

UZALISHAJI NA USINDIKAJI WA MAEMBE (DODOMA)

Mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) ni mradi wa kuendeleza sekta binafsi unaofadhiliwa na Danida. Mradi unashughulikia vikwazo vikuu vinavyokwamisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya wilaya kwenye mikoa miwili ya Dodoma na Kigoma nchini Tanzania. LIC imejikita katika mijadala kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miundombinu ya utoaji wa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na vituo vya pamoja vya biashara na miundombinu ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji. Washirika wanaotekeleza mradi wa LIC ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretariati za mikoa ya Kigoma na Dodoma, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Tanzania, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

Mwezi wa nne mwaka 2018, LIC ilisaini mkataba na **Mpunzugulu Agriculture and Marketing Cooperative Society Limited (MAMACOSO)** chini ya ushirikiano na wilaya ya Chamwino (mkoani Dodoma) kusaidia kuanzishwa kwa uzalishaji wa embe na kiwanda cha kusindika juisi ya embe.

Uzalishaji wa embe nchini Tanzania ni rafiki sana na kama ilivyo desturi unalimwa katika mfumo wa kuchanganya mazao na sio kulima zao la embe peke yake katika shamba kubwa ambapo kuna athari mbaya kwa viumbe hai na mazingira yao. Kuna soko liko tayari nchini Tanzania la embe, na tena maembe yanaonekana kuingizwa kutoka Kenya kuongezea uzalishaji wa ndani. Changamoto moja kuu, hata hivyo, ni msimu wa usambazaji na kukosekana kwa uwezo wa kusindika ili kukidhi uzalishaji uliozidi msimu wa mavuno mengi. Kiwanda cha usindikaji kitaongeza faida ya uzalishaji wa embe na kuruhusu wakulima wengi kukichukulia kilimo cha embe kwa mkazo zaidi na hivyo kuongeza maembe kitaifa.

MAMACOSO ni chama cha ushirika kilichosajiliwa kwa lengo kuu la kukuza uzalishaji na usindikaji embe. Ushirika una wanachama 200 wakiwemo wanawake 80 na wana jumla ya eneo lenye ekari 200. Ekari nyengine za nyongeza 500 zitanunuliwa chini ya ulimaji wa embe katika kujiandaa na kuanzisha kiwanda cha usindikaji. Mbali na uzalishaji wa juisi ya embe, mabaki pia yanaweza kutengenezea chakula cha wanyama.

Msaada wa LIC kwa MAMACOSO umegawanyika katika awamu tatu

Awamu ya kwanza (1)

- i. Kuandaa shamba, kupandikiza miche na kusambaza maji kwaajili ya umwagiliaji na usindikaji
- ii. Kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi na kutoa hati za kimila kwa wanachama wa MAMACOSO
- iii. Kuanzisha kampuni inayoitwa HUMACO Ltd kusimamia mradi ikijumuisha na kiwanda cha usindikaji

Awamu ya pili (2)

- i. Kujengea uwezo AMCO, Bodi na wanachama wa SACCOS
- ii. Kujenga nyumba mbili za maafisa kilimo na msimamizi wa uzalishaji

Awamu ya tatu (3)

- i. Kujenga kiwanda cha kusindika juisi ya embe
- ii. Ununuzi wa vifaa

Mambo muhimu na mafanikio

MAMOCOSO kupitia msaada wa LIC imeweza kupata mpango wa matumizi bora ya ardhi na hati za kimila kwa wanachama wake 175, umewezesha wanachama hawa kuingia mikataba na makubaliano ya mikopo na wasambazaji wa pembejeo na benki za biashara kwa kutumia hati za ardhi kama dhamana ya mkopo. Tanzania Agricultural Development Bank inaangalia ili kuweza kutoa mikopo mara baada ya mpango wa biashara kukamilika.

Mpango wa biashara unaandaliwa kukidhi mkakati wa uwekezaji biashara. Mpango biashara unaonyesha maeneo makubwa ya uwekezaji yenye faida za haraka, shughuli za biashara endelevu na usimamizi wa shamba na vifaa vya usindikaji kuwekezwa hapo baadaye. Hii itatoa ramani ya uwekezaji wa baadaye na pia kufanya kazi kama chombo usimamizi.



Shamba la maembe katika eneo la MAMACOSO

Fursa za ziada za ajira zinatengenezwa kupitia kuongezeka kwa uzalishaji wa embe na katika viwanda vya usindikaji. Mbali zaidi, uwekezaji huu unafungua fursa mpya za biashara katika kusaidia kazi za kiwanda cha embe na kiujumla zaidi katika kukuza shughuli za uchumi ndani ya eneo husika.



Uzalishaji wa miche ya miti ya miembe eneo la MAMACOSO

Bomba la maji katika eneo la MAMACOSO

Mpango wa awamu ya tatu ya ujenzi wa kiwanda cha usindikaji utaongeza thamani ya uzalishaji wa embe na kwa kiasi kikubwa kupunguza hasara baada ya mavuno. Hata hivyo, maembe halisi, vipande vya embe vilivyokaushwa na mchuzi wa maembe zinaonekana kama njia mbadala ya kupata juisi iliyosindikwa kutokana na embe. Ongezeko la thamani litaongeza uwekezaji katika upandaji wa miti ya miembe. Kuna wigo mpana wa ongezeko la thamani mbali na kuzalisha juice. Mabaki yake yanaweza kutumika kutengeneza chakula cha wanyama na pia yanaweza kutumika katika uzalishaji wa gesi asilia unaotokana na kinyesi cha wanyama na baadaye usambazaji wa nishati endelevu.

Tayari LIC imesaidia Mpunzugulu Agriculture and Marketing Cooperative Society Ltd kiasi cha shilingi milioni 81.4 katika awamu ya kwanza.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya mradi wa LIC: www.lic.or.tz